

# TAIFA LANGU NIMEKUTENDEA NINI?

By Enteshi Lukuliko.
Kahama Cathedral.
07 April 2025.

Ijumaa kuu.




1.Kwa ku wa nikutoa katika nchi ya Mi sri: Umemtayarishia Mwokozi wako M sa la ba.

2.Kwa kuwa nimekuongoza jangwani kwa miaka arobaini,na kukulisha kwa mana,na kukuingiza katika nchi nzuri sana: Umemtayarishia Mwokozi wako msalaba.

3.Ilinipasa kukutendea nini zaidi,nisikutendee? Kweli nimekupenda sana kama shamba langu zuri la mzabibu mwema sana: nawe umegeuka kuwa mche usiofaa wa mzabibu-mwitu machoni pangu: kwani nilipokuwa na kiu ulininywesha siki, na ulitoboa kwa mkuki ubavu wa Mwokozi.

4.Mimi kwa ajili yako niliipiga mijeredi Misri, pamoja na wazaliwa wake wa kwanza: nawe ukanitoa nipigwe mijeredi.

5.Mimi nilikutoa Misri, nikamtosa Farao katika Bahari ya Shamu:nawe ukanitoa kwa makuhani wakuu.

6.Mimi nimeifunua bahari mbele yako:nawe ukaufunua ubavu wangu kwa mkuki.

7.Mimi nilikuongoza mbele kwa mnara wa mawingu: nawe ukanipeleka ya Baraza la Pilato.

8.Mimi nilikulisha mana jangwani: nawe ukanipiga makofi kwa mijeredi.

9.Mimi nilikunywesha maji ya uzima yaliyotoka mwambani:nawe ukaninywesha nyongo na siki.

10.Mimi niliwapiga wafalme wa Kanaani kwa ajili yako: nawe ukanipiga kichwa changu kwa mwanzi.

11.Mimi nilikupa fimbo ya kifalme: nawe ukanivika taji la miiba kichwani.

12.Mimi nilikutukuza kwa uwezo mkubwa: nawe ukanitundika katika mti wa Msalaba.

Enteshi Lukuliko.
Normal call:+255 767 90 77 66.
WhatsApp call:+255 784 90 77 66.
Email:jumalukuliko6@gmail.com